

## WEB-PUBLICATION

### Note:

This is a web-publication. Please use as reference:

- Obure-Morang'a, Mark, Maud Devos & Inge Brinkman (eds.), 'Transcription of Swahili theatre play 'Nzala ya ndugu si mutu' by Kwale Arts Troupe' (VLIR-UOS Team project 'Storytelling and Young People Coping with Crisis: Oral Narratives and Crisis Management in Kenya and Ethiopia', 2023) <https://www.ol4d.ugent.be/>.

## Transcription of the Swahili theatre play

### 'Nzala ya ndugu si mutu'

### by Kwale Arts Troupe

Live performance in Kwale, Kenya, May 2023

Mkurugenzi wa filamu – Wakili Mwatondo  
Mkurugenzi msaidizi – Suleiman Madaraka  
Msimulizi, Babu – Juma Rang'ombe  
Mwagawari – Hussein Kaneno  
Mke wa Mwagawari – Jedidah Kimanzi  
Mwagamboga – Mohammed Madzambo  
Mtoto wa kwanza – Jedidah Kimanzi  
Mtoto wa pili – Mwanatibu Ndala  
Mtoto wa tatu – Fatuma Zani  
Baba – Mohammed Madzambo  
Kijana wa kwanza – Rama Mohammed  
Kijana wa pili – Swalehe Fungo  
Paka – Swalehe Fungo  
Binti wa Mwagamboga- Mwanatibu Ndala  
Dada anayeza - Jedidah Kimanzi

*(Watoto wanafika mahali pa kucheza)*

**Mtoto wa kwanza:** Here we are.

**Mtoto wa pili:** Mimi ndo nitaanza.

**Mtoto wa kwanza:** Naanza mimi.

**Mtoto wa tatu:** Aa. Cheza peke yako.

**Mtoto wa kwanza:** Cheza basi.

**Mtoto wa pili:** Nakwanzaa kiburugu.

**Mtoto wa tatu:** Cheza peke yako.

*(Mtoto wa pili na wa tatu wanaanza kucheza na kuimba)*

**(kwa pamoja) Naakwanzaa**

*Ba ba by show, I love you baby*

**Mtoto wa tatu:** *(akimsukuma mtoto wa kwanza, huku akimvuta mtoto wa pili ili wacheze naye)* Hujui nakwambia!

**Mtoto wa pili:** Si nawaambia.

*(Mtoto wa pili na wa tatu wanaendelea kucheza)*

**(kwa pamoja)** Ee kwanzaa

*Ba ba by show, I love you baby*

*the baby to the son, the son to the owner*

*the owner to the men, the men...*

*(Mtoto wa kwanza anataka kujiunga nao):* Nimechoka.

**Mtoto wa tatu na wa pili** *(kwa pamoja):* Haichezangwi watu watatu.

**Mtoto wa tatu:** Cheza pekee yako.

**Mtoto wa kwanza:** *(kwa huruma)* Nitaweza. Jamani.

**Mtoto wa pili na wa tatu:** Basi kaa hapa.

**(wote kwa pamoja)** *Ukuti ukuti,*

*wa nazi wa nazi*

*wenzetu wenzetu aligongwa na gari “adush”*

*Tumpeleke posta na anaanguka adush!*

*(Baba anajitokeza huku akiwaiga)*

**Watoto:** Baba, Baba.

**Baba:** Tumpeleke posta ananianguka adush! Eeh, Mnacheza *Ukuti ukuti!*

**Watoto:** Shikamoo.

**Baba:** Marahaba, marahaba. Sasa ngoja.

*(Wanamsaidia na mzigo)*

**Baba:** Sasa, ekeni, ekeni chini, ekeni chini tunacheza *ukuti! Ukuti!* Sasa.

**Watoto:** Baba utaangukaaaaa, hahaha!

**Baba:** Sianguki mimi, nilikua ninaruka kama Maasai.

**Watoto:** Aaya haya!

**Baba:** *Ukuti! Ukuti!*

**Mtoto wa pili:** Polepole usimwangushe, baba.

**Watoto:** *Wa mnazi wa mnazi!*

**Baba:** *Ukiruka Ukiruka.*

**Watoto:** Alianguka *adush!* Hahahaha.

**Baba:** Sasa mimi nawaambia.

**Mtoto:** Hahaha! Babaa.

**Baba:** Mimi nlikua makini katika haya mambo ya kurukaruka, kwanza mimi nachukua haya mahindi yangu nakuyaanika pale nyumbani na baadaye mumchunge kuku na mchukue myaponde. Sawa?

**Watoto:** Sawa, baba.

**Baba:** Mnanielewa?

**Watoto:** Sawa, baba.

**Baba:** *(kwa ucheshi)* *Ukuti ukuti!*

**Watoto:** *Wa mnazi wa mnazi!*

**Baba:** Akampeleke...

**Watoto:** *posta.*

**Baba:** Akampeleke...

**Watoto:** *posta.....*

**Baba:** Sawa.

*(Baba anaondoka)*

**Watoto:** Eeh, baba, safari njema.

**Baba:** Sawa.

**Mtoto wa pili:** Tucheze tena, haaha.

**Mtoto wa tatu:** Aah, nenda ukacheze pekee yako.

**Babu:** Watoto mambooooow!

**Watoto:** Poaaaah!

**Babu:** Mchapo waa liini?

**Watoto:** Keshoooo.

**Babu:** Ebu ringeni!

**Watoto:** Yeeeeh.

**Babu:** Ringeni tenaaa...hahaha.

**Babu:** Hadithi! hadithi!

**Watoto:** Hadithi njoooo, uongo njoo, tamu kolea kolea. Panya mdaku apigwe du du, ashatoroka uyoooo!

**Babu:** Asanteni sana, watoto wazuri.

Sasa zamani za kale katika kijiji cha Mwambara, paliishi ndugu wawili. Mwangamboga na Mwangawali. Katika kijiji hiki cha Mwambara, wakaazi wa Mwambara waliishi kwa raha na furaha na amani, mvua ilinyesha tena kwa wingi. Mazao shambani nayo, yakawa yanapatikana kwa wingi. Mifugo nayo ilikuwa ikizaana mara kwa mara hivyo basi waliokuwa wafugaji waliweza kuwa na mali nyiingi kwa kipindi cha kwa kipindi kifupi. Siku zilienda, wiki zikapita, miezi ikasonga, miaka ikapita hali ikaanza kubadilika. Kutoka kwenye furaha na mazao mengi hadi kwenye huzuni na vilio.

**Watoto:** Hihihihii.

**Babu:** Ukame ulitokea mifugo ikaanza kufa, mimea ikaanza kukauka, chemichemi za maji, maziwa na mito vyote vikakauka. Njaa iliumiza sana wanakijiji cha Mwambara, vijana nao wakaanza tabia ambazo hazikupendezesha wanajamii.

**Kijana wa kwanza:** Bwana, ukoaje mwanangu.

**Kijana wa pili:** Poa poa.

**Kijana wa kwanza:** Mbona haja [...]

**Kijana wa pili:** Njaa! Njaa mwanangu. Njaa.

**Kijana wa kwanza:** Komaa ee mwanaume ni *hustling* mwanangu.

**Kijana wa pili:** Nakomaa lakini hakuna chochote mtaani. Njaa, baba.

**Kijana wa kwanza:** Hata kama hakuna chochote, wewe hupambani, mwanaume ni kupambana na kujikakamua!

**Kijana wa pili:** Hakuna michongo siku hizi.

**Kijana wa kwanza:** Aaaah, tulia! Tulia mambo ya mchongo tulia mchongo mwenyewe huo.

(*Binti mmoja anayepita*)

**Kijana:** Dada, wewe!

**Dada:** Nini mbaya?

**Kijana wa kwanza:** Changamuka... Eti nini mbaya.

(*Wanamuangusha na kumpokonya kikapu alichokua akibeba*)

**Babu:** Watu kijijini waliachwa wakilalamika siku baada ya siku. Hali ikazidi kuwa mbaya kabisa kabisa. (**aaah, hihihii**) Siku Moja Mwangamboga hali ilikua ngumu zaidi na akaamua “mimi katika hali hii ni lazima nimwendee kaka yangu Mwangawari”. Mwangawari naye hakuwa maskini viile katika muda ule kwa sababu alikuwa miongoni mwa wale matajiri waliokuwa wakivuna chakula kingi kwa mpigo. Hivyo basi, wakati wengine wameanza kukumbwa na baa la njaa, Mwangawari alikuwa nacho japo kidogo katika gala lake.

**Mwangawari:** Niache, bwana!

**Babu:** Mwagawari alianza tabia zisizo za kawaida na akawa amemwamuru mke wake kupika mapema kabisa kabla ya giza litande, ifikapo usiku jikoni pasiwe na moto kabisa. Lakini Mwagamboga ... Mwagawari na mkewe walikuwa na tabia moja ama walikuwa na hila moja, hila hii ilikuwa uroho na uchoyo.

**Mwagawari:** Wewe mke wangu!

**Mke:** Naam.

**Mwagawari:** Vipi? Chakula tayari?

**Mke:** Ndio.

**Mwagawari:** Haa sasa njoo, njoo huko njoo. Sasa unajua simama hapa bwana, sasa hapa wajua njama ni ile ile, sheria ni ile ile! Tunachukua chakula saa hii, tunakula hapa, atakayekuja hakuna chakula. Hayaa fanya mambo yako. (*Wananawa mkono*) Heee! Mke wangu, nakupenda wewe.

**Mke:** Nakupenda pia!

**Babu:** Siku moja, Mwagawari alipokua anapata chajio, ama chakula cha usiku, pamoja na mke wake, kaka yake Mwagamboga alikuwa hali imemzidi na akawa hawezi kustahimili tena. Ilimbidi Mwagamboga akatoka kwake nyumbani kumwendea kaka yake Mwagawari ili akapate kuomba msaada japo tu kikombe cha unga akawatayarishie wanawe uji waweze kulala.

(*Wanasikia hodi mlangoni wanajipanguza midomo, kisha wanaficha chakula*)

**Mwagamboga:** Hodi hodi Mwagawarii?

**Mwagamboga:** Mwenyewe huku!

**Mwagawari:** Yaani?

**Mwagamboga:** Mwagamboga?

**Mwagawari:** Ah, ngoja kidogo, nreta, nreta, nreta, nchooni, bwana! Naja, naja! Aaah, habariyo bwana, habari yako bwana?

**Mwagamboga:** Nsalama bwana.

**Mwagawari:** Karibu bwana, karibu *bro*, karibu nyumbani kakangu.

**Mwagamboga:** Asante sana, asante sana.

**Mwagawari:** Karibu nyumbani.

**Mwagamboga:** (*huku akishikilia tumbo*) Mfungu huu bwana ee ...Habari shemeji? Salaama shemeji?

**Mwagawari:** Salaama?

**Mke:** Salama.

**Mwagamboga:** Huku kwenu kama kuko salama mimi kule kwangu hakuko salama! Kutoka jana, watu wanaangalia paa tu hatujakula. Hivi ninavyowaambia watoto wako hapo wameanguka libata nikaamua afadhali nije hapa ndio nangaa kama una kauji ka-kaunga kauji kidogo nikawafanyie muswa ndio nao pia wapate la ukana.

**Mke:** Huku kwetu hakuna kitu!

**Mwagawari:** Unaona, Unasikia mke wangu anayasema, yeye ndiyo mambo ya jikoni, mimi hata siusiki! na yeye amesema ndugu yangu hapa nyumbani hali ni ngumu, ile hali ilioko kule kwako hata hapa pangu iko ni iyo iyo hali ngumu.

**Mwagamboga:** Angalia angalia bwana!

**Mwagawari:** Hakuna chakula, si unamskia hata shemeji yako anakuambia hakuna chakula, kama hakuna chakula bwana.

**Mwagamboga:** Okey

(*Babu anaendelea na hadithi*)

**Babu:** Ama kweli, hii ilikua *njaa ya ndugu si mutu*. Kwa kuwa hata wale ndugu waliopendana, ule udugu wao ulikuwa tayari kukatika kwa sababu ya chakula ama ukosefu wa chakula. Mwagamboga alijaribu sana kumsihi kaka yake aweze kumsaidia japo tu kikombe cha uji kikombe cha unga ili

akawapikie wanawe uji lakini juhudi zake hazikuweza kufaulu (**Mwagamboga:** Kidogo tu).  
Mlango ulikuwa wazi paka naye alionekana akiingia na kunesanusa kuelekea mvunguni.

**Paka:** meow, meow, meow, meow, meow!

**Mwagawari:** Bobi, bobi, bobi, bobi, bobi!

**Paka:** Meow!

**Mke wa Mwagawari:** Bobi, bobi!

**Paka:** Meow.

**Mwagawari:** Bobi, Bobi.

**Paka:** Meow.

**Mwagawari:** Bobi! Unaenda wapi wewe, paka huku? Wewe paka, unaenda wapi, paka huku tu? Ebu Rudi, rudi, rudi tu! Rudi nyumba yangu, rudi nyamaa yangu!

**Babu:** Ghafla bin vuu, paka yule aliwapita akaingia mvunguni alitoka na kipande cha kuku mdomoni, akatoka mbio. Mwagawari kuona vile hakukubali aliamua kumfuata paka. “Taka nyama yangu, nipe nyama yangu, nipe nyama yangu! wewe paka, wewe paka leta nyama yangu leta nyama yangu!”

Wakafukuzana huku kote. Paka mbele, Mwagawari nyuma “nataka nyama yangu! nataka nyama yangu!” Paka alikimbia moja kwa moja mpaka nyumbani kwa jirani, akaingia ndani, Mwagawari naye kwa kuwa alikuwa nyuma akimwandama paka naye akafululiza ndani, paka akatoka kupitia dirishani. Mwagawari akasema “Ahaa! Dirishani tu!” naye akaruka choo [...] dirishani akatokea upande wa pili. Wakafukuzana huko “nyama yangu! nyama yangu! nataka nyama yangu!” Toka paka yuko mbele, Mwagawari yuko nyuma, mpaka ndipo Mwagawari alikua mbele, paka akawa nyuma. “Nataka nyama yangu! Nataka nyama yangu!” Baada ya jitihada zote, Mwagawari hakufaulu na ilimlazimu arudi nyumbani bila kuipata nyama yake. Alirudi nyumbani akiwa amechoka, ana hasira, ana njaa, hajala nyama ilikuwa ile ile na paka ameenda nayo.

**Mwagawari:** Wafanya nini hapa weewe?

**Mwagamboga:** Sasa wewe.

**Mwagawari:** Nenda kwako huko!

**Mwagamboga:** Kumbe kumbe hata chakula ulikua nayo!

**Mwagawari:** Quii....Quiet, quiet, stop, stop [...]! Kwenda zako uko! Wewe ndiye unakuja kunaleta kiherehere mpaka nyama yangu inaondoka na kuku.

**Mke:** (*kwa ukali huku akimnyoshea kidole*) Wewe ndiye umesababisha haya yote, toka! Toka.

**Mwagamboga:** Shemeji na...

**Mke:** Toka, toka, toka!

**Mwagawari:** Nenda, nenda, nenda, nenda.

**Babu:** Wakati Mwagawari na Mwagamboga wanalumbana, sauti ya kilio ilisikika kwa mbali sana

**Mke:** Toka, toka, mlango ni ule get out toka now.

**Binti:** Uuui, haaaaaa. Hiiiihihi. Hiiii, babaaa! babaaaa! babaaaa! Aaaaha, Babamboga! Babamboga Kufaaaaahaha!

**Babu:** Wote wakaelekeza nyuso zao kulikokuwa kunatokea kilio kile. Kufumba na kufumbua, kilio kilikuwa cha bintiye Mwagamboga. (*Bintiye Mwagamboga anaendelea kulia*)

**Binti:** Baba amekufaa!

**Mwagamboga:** Amekufa! Aa. Amekufa! A.

**Babu:** Hapo ndipo ilipobainika ya kwamba, mtoto wa Mwagamboga aliyekuwa akilia njaa nyumbani pamoja na mwenzake alikuwa amefariki dunia. Ndugu hao wawili walilaumiana wasijue cha kufanya na hatimaye hadithi ile ikiishia palepale.